# HATI YA MAKUBALIANO YA KUHAMISHA UMILIKI WA KISIWA.

**(KILICHOPO ENEO LA NYAMIYUGUYU, MTAA WA IHUMILO, KATA YA LUCHELELE NDANI YA HALMAHSAURI YA JIJI LA MWANZA)**

Hati hii imeandaliwa na kusainiwa hapa MWANZA, leo tarehe __17__ Mwezi __07__ 2023

**BAINA YA**

**PAUL JAMES MATIKO** wa **S.L.P 7575 MWANZA, SIMU NAMBA: 0767684211** (ambaye hapo baadaye lengo la makubaliano haya, atarejewa kama "**Mmiliki wa awali**" ikijumuisha warithi wake, ndugu zake, wakala wake au mtu yeyote anayefanya kazi kwa maelekezo yake) kuwa upande mmoja wa makubaliano haya.

**AND**

**KIJIJI DUNIA UNIQUE LIMITED** wa **S.L.P 1767 MWANZA** (ambayo hapo baadaye itarejewa "**Mmiliki mpya**" ikijumuisha wakurugenzi wake, uongozi au mtu mwingine yeyote anayefanya kazi kwa maelekezo yake) kuwa upande wa pili wa makubaliano haya.

**KWA KUWA:** Mmiliki wa awali ni mtu binafsi, Mtanzania, akiwa na akili timamu na akiwa ndiye mmiliki halali wa Kisiwa hiki kilichopo **NYAMIYUGUYUGU, Mtaa wa IHUMILO**, Kata ya **LUCHELELE, Halmashauri ya Mwanza** (ambacho baadaye katika hati hii kitarejewa kama "**Kisiwa**). Na kuwa ni mmoja kati ya wakurugenzi wa **KIJIJI DUNIA UNIQUE** (ambayo pia yaweza kurejewa kama "**Kampuni**". Kwa kuzingatia misingi na masharti ya makubaliano haya, anayo nia ya kuhamisha umiliki wake katika Kisiwa hiki kwenda kwa Mmiliki mpya.

**NA KWA KUWA:** Mmiliki mpya ni Kampuni iliyosajiliwa chini ya sheria ya Makampuni ya Tanzania (**Companies Act Cap 212**), akiwa na uhalali wa kumiliki na kuuza mali zake kwa jina lake, na kupitia azimio la Bodi ya wakurugenzi wake na uongozi wake wanakubali kwa masharti na misingi iliyowekwa kwenye hati kupokea umiliki wa Kisiwa hiki.

**NA KWA KUWA:** Kwa kuzingatia maslahi mapana ya pande zote mbili kwa lengo la kuiongezea nguvu ya utendaji kazi ndani ya Kampuni pande zote mbili kwa nia moja

wamekubaliana kuhamisha umiliki wa Kisiwa hiki kutoka kwa mmiliki wa awali kwenda kwa mmiliki mpya kwa kuzingatia masharti na misingi inasomeka ndani ya hati hii.

**HIVYO BASI**: Kama ushahidi wa kile kilichokubaliwa katika hati hii, makubalisho haya yanashuhudia kama ifuatavyo:

1. Kwamba, mmiliki wa awali anahamaisha umiliki wake pamoja na haki zake zote katika kisiwa hiki kwenda kwenye jina la mmiliki mpya, ikiwa ni jumla ya malipo ya Hisa zake zote ambazo ni **45% ( sawa na Hisa 4500)** ya Hisa zote, na malipo ya Hisa zote za mtoto wake **MOSES PAUL KASSINGA** mwenye **5% ( sawa na Hisa 500 )** ya Hisa zote. Hivyo mmiliki mpya hana madai yoyote halali kuhusiana na Hisa tajwa kuwa wamiliki hawa wawili wana uhalali wa Hisa zao. Kwa misingi hii kwa sasa Hisa hizo ni mali yao binafsi.

2. Kwamba, Mmiliki mpya anakubali kupokea uhamishaji wa miliki kwenda kwenye jina lake, na kuwa Kisiwa hiki ni mali ya Kampuni kwa ajili ya shughuli za Kampuni na hivyo kwa kusaini hati hii mmiliki wa awali amefikia ukomo wake umiliki wake isipokuwa kama ilivyoelezwa ndani ya Nyaraka za uanzishwaji wa Kampuni (Memorandium of Association and Articles of Association)

3. Kwamba, kuanzia sasa mmiliki mpya ataendelea na mchakato wa upatikanaji wa hati miliki **(Certificate of Title)** kwa jina lake na kwa kutumia gharama zake na kuwa mmiliki wa awali yuko tayari muda wowote baada ya kupewa taarifa kwa njia sahihi kutoa ushirikiano ili kukamilisha zoezi hili.

4. Kwamba, Kuanzia siku ya kusainiwa kwa makubaliano haya, mmiliki wa awali ana umiliki kamili ya Hisa zake zote pamoja na mwanae na hivyo wana haki zote ndani ya Kampuni, na wanapaswa kufurahia haki zao ikiwa ni pamoja na kupewa gawio kwa kiwango cha Hisa zao zote baada ya utaratibu waliokubaliana kukamilika na kwa kuzingatia taratibu za Kampuni.

5. Kwamba, mmiliki wa awali anatamka kuwa Kisiwa hiki ni mali yake binafsi na kuwa hakuna mtu mwingine mwenye maslahi halali au madai halali katika Umiliki wa Kisiwa hiki, iwe ndugu zake, mke/wake zake wala hakijawekwa rehani kama dhamana ya mkopo katika taasisi yoyote. Endapo itathibitika kuwa kinyume basi

mmiliki wa awali atawajibika kumaliza madai hayo bila kuathiri umiliki wa Mmiliki mpya.

6. Endapo kutajitokeza mgogoro wa aina yoyote, pande zote mbili zitachukua hatua za makusudi kumaliza mgogoro wao kwa njia ya Amani kabla ya kuchua hatua za kisheria kwa kuchagua msuluhishi ambaye anakubalika kwa pande zote mbili au katika chombo ambayo watakichagua wako kwa ajili ya zoezi hili.

7. Endapo zoezi la kumaliza mgogoro kwa njia ya amani litashindikana, upande unaohisi kuwa unaonewa utakuwa na haki ya kuchukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kwenda Mahakamani au kwenye chombo chochote chenye mamlaka ya kusikiliza migogoro ya aina hii.

8. Makubaliano haya, yanatafsiriwa na kusimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mikataba (**The Law of Contract of Tanzania Cap 345 R.E 2019), Sheria ya Ardhi (the Land Act, Cap 113 R.E)** pamoja na sheria nyinginezo zinazosimamia miliki ya usajili wa Ardhi na kwa muda wote sheria za Tanzania zitatumika.

**IMESAINIWA** na **KUPOKELEWA** hapa **MWANZA** na **PAUL JAMES MATIKO** ninayemfahamu binafsi / ametambulishwa Kwangu na **GEOFREY MEDARD LUTENTA** ninayemfahamu Katika uwepo wangu, tarehe 17 Mwezi 07 2023

______________
**MMILIKI WA AWALI**

**MBELE YANGU:**

**JINA:** MSALABA KAUNDA BERNARD

**SAINI:** ______________

**ANUANI:** S.L.P 2957 MWANZA

**WADHIFA:** WAKILI

**TAREHE:** 17.07.2023

Msalaba Kaunda Bernard
Box 2957 Mwanza
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

**IMESAINIWA na KUPOKELEWA** hapa **MWANZA**
Kwa niabaya ya **KIJIJI DUNIA UNIQUE LIMITED** na
**ELPIDIUS FRANK MPANJU** ambaye ametambulishwa
kwangu na **GEOFREY MEDARD LUTENTA**
tarehe 17 Mwezi 07 2023

**MMILIKI MPYA**

KIJIJI DUNIA UNIQUE LIMITED
P.O. Box 1767
MWANZA

**MBELE YANGU:**

**JINA:** MSALABA KAUNDA BERNARD

**SAINI:**

**ANUANI:** S.L.P 2957 MWANZA

**WADHIFA:** WAKILI

**TAREHE:** 17.07.2023

Msalaba Kaunda Bernard
Box 2957 Mwanza
Advocate, Notary Public
& Commissioner for Oaths